# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 993

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Elimu ya Msingi Darasa la I na la II

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-815-6

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Elimu ya Msingi Darasa la I na la II Tanzania Bara.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA ELIMU YA MSINGI DARASA LA I NA LA II

**2023**

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza 2023

ISBN: 978-9987-09-815-6

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es Salaam

Simu: +255 735 041168 / 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Muhtasari wa Elimu ya Msingi Darasa la I na II.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

## Yaliyomo


Orodha ya majedwali ........ iv
Vifupisho ........ v
Shukurani ........ vi
1.0 Utangulizi ........ 1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania ........ 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la I na la II ........ 2
4.0 Umahiri wa jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la I na la II ........ 2
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ........ 3
6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 4
6.1 Mwalimu ........ 5
6.2 Mwanafunzi ........ 5
6.3 Mzazi/mlezi ........ 6
7.0 Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji ........ 6
8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 6
9.0 Upimaji ........ 7
10.0 Idadi ya Vipindi ........ 7
11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 8
Darasa la I ........ 8
Darasa la II ........ 8
Bibliografia ........ 33

## Orodha ya majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Mahususi kwa Darasa la I na la II ........ 3

Jedwali Na. 2: Mgawanyo wa Muda na Vipindi Darasa la I na la II kwa Wiki ........ 8

Jedwali Na. 3: Maudhui ya Darasa la I ........ 9

Jedwali Na. 4: Maudhui ya Darasa la II ........ 21

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| LAT | Lugha ya Alama ya Tanzania |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| WyEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |

# Shukurani

Maandalizi ya muhtasari wa Elimu ya Msingi Darasa la I na la II yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha kupatikana kwa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala. Vilevile, TET inaishukuru Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la Uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Muhtasari huu una umahiri sita za lazima kwa mwanafunzi anayesoma elimu ya msingi darasa la I na la II kwa kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Umahiri hizo ni Kusoma, Kuandika, Kuhesabu, Demontsrate Mastary of Basic English language Skills, Kuthamini Utamaduni, Sanaa na Michezo, na Kutunza Afya na Mazingira. Aidha, umahiri hizo zina maudhui yanayolenga kumwezesha mwanafunzi kujifunza stadi za awali za utumiaji wa programu za kompyuta. Lengo kuu la kujifunza umahiri hizi ni kukuza stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK), kujenga uelewa wa awali wa lugha ya Kiingereza na kujenga stadi nyingine za utamaduni, sanaa, michezo, afya na mazingira zitakazomsaidia mwanafunzi kumudu maisha yake ya kila siku. Aidha, umahiri hizi pia zinalenga kujenga uelewa wa awali wa utumiaji wa programu za Kompyuta. Stadi hizi ni msingi muhimu katika kumwezesha mwanafunzi kujifunza kwa ufanisi na kumudu ujifunzaji wake katika ngazi za juu.

Muhtasari wa Elimu ya Msingi Darasa la I na la II umeandaliwa kwa lengo la kumwongoza mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa umahiri sita zilizoainishwa katika muhtasari kwa shule zinazotumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia Tanzania Bara. Muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Elimu ya Msingi wa Mwaka 2023. Muhtasari utamwezesha mwalimu kupanga shughuli za ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, muhtasari huu unasisitiza matumizi ya mbinu zitakazomwezesha mwanafunzi kukuza stadi za Karne ya 21 zikiwemo kufikiri kimantiki, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa matatizo.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;
(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la I na la II

Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la I na la II ni kumwezesha mwanafunzi:

(a) Kukuza stadi za Kusoma, Kuandika, na Kuhesabu (KKK), ikihusisha kutumia maandishi ya breli, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;
(b) Kukuza uwezo wa kuwasiliana kwa njia stahiki ikiwemo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na teknolojia saidizi;
(c) Kujenga uimara wa mwili, kukuza vipaji, kushirikiana na wenzake na kuwa na mtazamo chanya kuhusu kujifunza;
(d) Kukuza urazini na ujumi, kupenda na kutunza afya na mazingira pamoja na rasilimali zilizopo;
(e) Kukuza maadili na uwezo wa kuthamini na kudumisha tunu za taifa na utamaduni wa jamii yake pamoja na kutambua tofauti za tamaduni mbalimbali; na
(f) Kukuza uwezo wa kuchangamana katika mazingira jumuishi.

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la I na la II

Umahiri wa jumla utakaojengwa na mwanafunzi wa Darasa la I na la II ni:

(a) Kutumia stadi za Kusoma, Kuandika, na Kuhesabu (KKK), ikihusisha kutumia maandishi ya Breli, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;
(b) Kuwasiliana kwa njia stahiki ikiwemo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na teknolojia saidizi;
(c) Kushiriki katika vitendo vya kuimarisha mwili, kukuza vipaji, kushirikiana na wenzake na kuwa na mtazamo chanya kuhusu kujifunza;

(d) Kuonesha urazini na ujumi, kupenda na kutunza afya na mazingira pamoja na rasilimali zilizopo;

(e) Kuonesha maadili, kuthamini na kudumisha tunu za taifa na utamaduni wa jamii yake pamoja na kutambua tofauti za tamaduni mbalimbali; na

(f) Kuchangamana katika mazingira jumuishi.

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Muhtasari wa Elimu ya msingi kwa Darasa la I na la II una umahiri mkuu na umahiri mahususi kama inavyojitokeza katika Jedwali Na.1.

**Jedwali Na. 1:** *Umahiri Mkuu na Mahususi kwa Darasa la I na la II*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kusoma | 1.1 Kutambua sauti za herufi<br>1.2 Kutambua uhusiano wa sauti na herufi<br>1.3 Kusoma kwa ufasaha<br>1.4 Kusoma na kusikiliza kwa ufahamu |
| 2.0 Kuandika | 2.1 Kumudu misingi ya kuandika<br>2.2 Kumudu stadi za kuandika<br>2.3 Kutumia kanuni za uandishi |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 3.0 Demonstrate mastery of basic English language skills | 3.1 Develop listening and speaking skills in different contexts<br>3.2 Develop early literacy and numeracy skills<br>3.3 Communicate in different contexts |
| 4.0 Kuhesabu | 4.1 Kutambua dhana ya namba<br>4.2 Kutumia matendo ya kihisabati<br>4.3 Kutumia dhana za kihisabati |
| 5.0 Kuthamini utamaduni, sanaa na michezo | 5.1 Kuthamini utamaduni wake na wa watu wengine<br>5.2 Kuheshimu tofauti za kiimani<br>5.3 Kuonesha matendo yenye maadili<br>5.4 Kubuni kazi za sanaa<br>5.5 Kushiriki katika michezo mbalimbali |
| 6.0 Kutunza afya na mazingira | 6.1 Kutunza afya yake na jamii inayomzunguka<br>6.2 Kuchunguza vitu vilivyomo katika mazingira<br>6.3 Kujilinda na mazingira hatarishi<br>6.4 Kutunza mazingira<br>6.5 Kuwa na mtazamo chanya kuhusu mazingira |

## 6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ujifunzaji na ufundishaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi/mlezi katika kutekeleza majukumu mbalimbali. Majukumu yao ni kama yafuatayo:

### 6.1 Mwalimu

Mwalimu anatarajiwa:

(a) Kumwezesha mwanafunzi kujenga umahiri uliokusudiwa;

(b) Kuandaa mazingira salama, rafiki na wezeshi ya kufundishia na kujifunzia;

(c) Kutengeneza au kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;

(d) Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji;

(e) Kuhakikisha kuwa ujifunzaji na ufundishaji unafanyika kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;

(f) Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo;

(g) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;

(h) Kumlinda mwanafunzi awapo shuleni;

(i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;

(j) Kubaini mahitaji ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki;

(k) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika malezi na ujifunzaji wa mwanafunzi; na

(l) Kuchopeka masuala mtambuka na TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 6.2 Mwanafunzi

Mwanafunzi anatarajiwa:

(a) Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa ili kupata umahiri unaokusudiwa;

(c) Kushirikiana na wenzake pamoja na mwalimu katika mchakato wa ujifunzaji; na

(d) Kuzingatia kanuni na taratibu za shule.

### 6.3 Mzazi/Mlezi

Mzazi mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi katika ujifunzaji;
(b) Kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma pale inapowezekana;
(c) Kufuatilia mwenendo wa kitabia wa mwanafunzi;
(d) Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayowezesha ujifunzaji;
(e) Kumpatia mwanafunzi vifaa vinavyotumika katika shughuli ya ujifunzaji;
(f) Kuhakikisha mwanafunzi anapata mahitaji muhimu; na
(g) Kumfundisha mtoto umuhimu na thamani ya elimu na kazi pamoja na kumuhimiza kujifunza kwa bidii.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Ujifunzaji na ufundishaji katika Darasa la I na la II utazingatia ujenzi wa umahiri unaotumia mbinu zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji na mwalimu kuwa mwezeshaji. Mwalimu atatumia mbinu zinazomshirikisha mwanafunzi katika tendo zima la ujifunzaji na ufundishaji kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai na uwezo wa mwanafunzi. Mbinu hizo ni za ujifunzaji shirikishi unaomwezesha mwanafunzi kufikiri, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali, majadiliano katika vikundi na kushiriki katika kutoa mrejesho. Baadhi ya mbinu hizo ni ziara za kimasomo, kazimradi na kazi nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujifunzaji.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Zana za ujifunzaji na ufundishaji zinapaswa kuwa shirikishi na zinazokidhi mahitaji, umri na uwezo wa mwanafunzi. Mwalimu anapaswa kuhakikisha mwanafunzi anapata nafasi ya kuona, kusikia na kushika zana. Aidha, zana za ujifunzaji na ufundishaji zinapaswa zimsaidie mwanafunzi kuelewa kinachofundishwa. Mwalimu anashauriwa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yanayomzungumka. Orodha ya vitabu vitakavyotumika vitatolewa na TET.

## 9.0 Upimaji

Upimaji ni suala muhimu katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji ili kuwezesha ujenzi wa umahiri unaokusudiwa. Upimaji wa darasa la I na la II utajumuisha upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji na utamwezesha mwalimu kubaini uwezo na uhitaji wa mwanafunzi katika ujifunzaji. Vilevile, utalenga kupima mabadiliko katika maarifa, stadi na mwelekeo wa kutenda, kuthamini, kusimulia na kutumia stadi anazojifunza katika mazingira yanayomzunguka. Aidha, mwalimu atatumia taarifa za upimaji kuboresha ufundishaji na kumwezesha mwanafunzi kufikia lengo la ujifunzaji. Zana za upimaji zinazoweza kutumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji ni bunguabongo, orodha hakiki, mazoezi ya darasani, majaribio, majaribio kwa vitendo, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi na zana nyingine kama hizo.

Upimaji tamati utahusisha mitihani ya wiki, mwezi, muhula na mtihani wa mwisho wa mwaka ambayo itatumika kupima maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi. Taarifa za upimaji huu pamoja na kutumika kutathimini maendeleo ya mwanafunzi, zitatumika kutoa mrejesho wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji.

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Elimu ya Msingi Darasa la I na la II unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ujifunzaji na ufundishaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za ujifunzaji. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 30. Idadi ya vipindi kwa kila umahiri ni kama ulivyooneshwa katika Jedwali Na. 2:

**Jedwali Na. 2:** *Mgawanyo wa Muda na Vipindi Darasa la I na la II kwa Wiki*

| **Umahiri** | **Idadi ya Vipindi** |
|---|---|
| Kusoma | 8 |
| Kuandika | 5 |
| Kuhesabu | 7 |
| Demonstrate Mastery of Basic English Language Skills | 6 |
| Kutunza Afya na Mazingira | 2 |
| Kuthamini Utamaduni, Sanaa na Michezo | 2 |
| **Jumla ya idadi ya vipindi kwa wiki** | **30** |

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Maudhui yamepangiliwa katika vipengele sita, ambavyo ni; Umahiri mkuu, Umahiri mahususi, Vigezo vya upimaji, Shughuli za ujifunzaji, Vifaa/zana na Idadi ya vipindi kama inavyojitokeza katika Jedwali Na.3 na 4.

**Darasa la I**

**Jedwali Na. 3:** *Maudhui ya Darasa la I*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kusoma | 1.1 Kutambua sauti za herufi | (a) Kubaini sauti za irabu (a, e, i, o, u) katika maneno | Sauti za irabu zimebainishwa (a, e, i, o, u) katika maneno | Kadi na chati za picha za vitu vinazoanza na irabu, kadi, chati na picha za irabu, maneno, vitu halisi, sauti za irabu na maneno yaliyorekodiwa | 37 |
| | | (b) Kuunganisha sauti za irabu ili kuunda maneno (oa, au, ua) | Sauti za irabu zimeunganishwa ili kuunda maneno (oa, au, ua) | | |
| | | (c) Kutambua sauti za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch) kwenye maneno | Sauti za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch) kwenye maneno zimetambuliwa | | |
| | | (d) Kutambua herufi kubwa na ndogo | Herufi kubwa na ndogo zimetambuliwa | | |
| | | (e) Kuunganisha sauti za konsonanti na irabu ili kuunda silabi | Sauti za konsonanti na irabu zimeunganishwa ili kuunda silabi | | |
| | | (f) Kutenganisha kwa kutamka sauti za konsonanti na irabu zilizounda silabi na silabi zilizounda maneno | Sauti za konsonanti na irabu zilizounda silabi na silabi zilizounda maneno zimetenganishwa kwa kutamka | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (g) Kutambua sauti za herufi mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw) kwenye maneno | Sauti za herufi mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw) kwenye maneno zimetambuliwa | | |
| | | (h) Kuunganisha sauti za herufi mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw) na irabu ili kuunda silabi | Sauti za herufi mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw) zimeunganishwa ili kuunda silabi | | |
| | 1.2 Kutambua uhusiano wa sauti na herufi | (a) Kuhusianisha sauti na herufi za irabu (a, e, i, o, u) katika matini | Sauti na herufi za irabu (a, e, i, o, u) katika matini zimehusianishwa | Kadi na chati za picha na herufi, ubao, maneno, video zenye sauti na majina ya herufi za irabu, sauti za irabu na maneno yaliyorekodiwa | 32 |
| | | (b) Kuhusianisha sauti na herufi za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch) katika matini | Sauti na herufi za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch) zimehusianishwa katika matini | | |
| | | (c) Kuhusianisha sauti na herufi za konsonanti mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw) katika matini | Sauti na herufi za konsonanti mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw) zimehusianishwa katika matini | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kuunganisha sauti za herufi za konsonanti mwambatano na irabu ili kusoma silabi katika makundi yote (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw) | Sauti za herufi za konsonanti mwambatano na irabu ili kusoma silabi katika makundi yote (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw) zimeunganishwa | | |
| | | (e) Kuunganisha silabi ili kusoma maneno | Silabi zimeunganishwa ili kusoma maneno | | |
| | | (f) Kutenganisha kwa kutamka sauti mojamoja ili kuunda maneno | Sauti zimetenganishwa kwa kutamka sauti mojamoja ili kuunda maneno | | |
| | | (g) Kuunganisha maneno ili kusoma sentensi | Maneno yameunganishwa ili kusoma sentensi | | |
| | 1.3 Kusoma kwa ufasaha | (a) Kusoma kwa sauti kifungu cha habari/ hadithi linganifu kwa kuzingatia matamshi sahihi ya maneno | Kifungu cha habari/hadithi linganifu kwa kuzingatia matamshi sahihi ya maneno kimesomwa kwa sauti | Kadi na chati za maneno, matini, picha za vitu mbalimbali na vifungu vya habari au hadithi zilizorekodiwa | 20 |
| | | (b) Kusoma kwa sauti kifungu linganifu cha habari/hadithi kwa kasi stahiki (maneno 40 kwa dakika) | Kifungu linganifu cha habari/hadithi kimesomwa kwa sauti na kwa kasi stahiki (maneno 40 kwa dakika) | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kusoma kwa sauti kifungu linganifu cha habari/hadithi kwa hisia na kwa kuzingatia alama za uandishi *(nukta, mkato, alama ya kuuliza na alama ya mshangao)* | Kifungu linganifu cha habari/hadithi kimesomwa kwa sauti, hisia na kwa kuzingatia alama za uandishi *(nukta, mkato, alama ya kuuliza na alama ya mshangao)* | | |
| | 1.4 Kusoma na kusikiliza kwa ufahamu | (a) Kutafsiri na kuelezea picha | Picha zimeelezewa na kutafsiriwa kwa usahihi | Kadi na chati za picha za vitu mbalimbali, matini ya habari/hadithi, hadithi/habari zilizorekodiwa | 21 |
| | | (b) Kubashiri maudhui ya habari/hadithi kwa usahihi kwa kutumia picha, jina la habari/hadithi na msamiati uliochaguliwa | Amebashiri maudhui ya habari/hadithi kwa kwa kutumia picha, jina la hadithi na msamiati uliochaguliwa | | |
| | | (c) Kusikiliza habari/hadithi kwa ufahamu | Habari/hadithi imesikilizwa kwa ufahamu | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kuandika | 2.1 Kumudu misingi ya kuandika | (a) Kutumia stadi za awali za kuandika | Stadi za awali za kuandika zimetumika | Kadi za herufi, viandikio, video zinazoonesha misingi ya kuandika | 14 |
| | | (b) Kuchora michoro ya herufi | Michoro ya herufi imechorwa | | |
| | | (c) Kufuatisha herufi kwa kuzingatia hatua | Herufi zimefuatishwa kwa kuzingatia hatua | | |
| | 2.2 Kumudu stadi za kuandika | (a) Kuandika herufi ndogo za irabu (a, e, i, o, u), konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch) kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua | Herufi ndogo za irabu (a, e, i, o, u), konsonanti (b, m, k, d, n) ; (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch) zimeandikwa kwa mpangilio kwa kufuata hatua | Kadi za herufi, video zinazoonesha namna ya kuandika herufi ndogo za irabu na konsonanti kwa mpangilio kwa kufuata hatua | 22 |
| | | (b) Kuandika herufi kubwa za irabu (A, E, I, O, U), konsonanti (B, M, K, D, N); (L, T, P, S, F, J); (G, Y, Z, H, R, W, V, CH) kwa mpangilio na kufuata hatua | Herufi kubwa za irabu (A, E, I, O, U) na konsonanti (B, M, K, D, N); (L, T, P, S, F, J); (G, Y, Z, H, R, W, V, CH) zimeandikwa kwa mpangilio na kufuata hatua | | |
| | | (c) Kuandika herufi mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw) | Herufi mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw) zimeandikwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kuandika silabi zinazotokana na herufi za konsonanti na irabu | Silabi zinazotokana na herufi za konsonanti na irabu zimeandikwa | | |
| | | (e) Kuandika silabi za herufi mwambatano | Silabi za herufi mwambatano zimeandikwa | | |
| | | (f) Kuandika sentensi fupi | Sentensi fupi zimeandikwa | | |
| | 2.3 Kutumia kanuni za uandishi | Kubaini alama za uandishi *(nukta, mkato, alama ya kuuliza na alama ya mshangao*) | Alama za uandishi *(nukta, mkato, alama ya kuuliza na alama ya mshangao*) zimebainishwa | Alama za uandishi zilizorekodiwa, matini zinazoonesha alama za uandishi na kadi/chati zinazoonesha alama za uandishi | 12 |
| 3.0 Demonstrate mastery of basic English language skills | 3.1 Develop listening and speaking skills in different contexts | (a) Imitate different sounds (eg. Sounds of animals, hand clap etc) | Different sounds are imitated (eg. Sounds of animals, hand clap etc) | Pictures, word lists, wall charts, audial/audio-visual materials | 30 |
| | | (b) Relate words with familiar objects found in the environment | Words are related with objects in the familiar environment | | |
| | | (c) Follow simple instructions given at school and home (e.g. go out, stand up, jump, clap your hands, touch your head and sit down) | Simple instructions given at school and home are followed | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Name parts of the body orally | Parts of the body are named orally | | |
| | 3.2 Develop early literacy and numeracy skills | (a) Pronounce English letter sounds (a-z) | English letter sounds (a-z) are pronounced | Wall chats, letter cards, real objects and audial/audio-visual materials | 40 |
| | | (b) Recognise English sounds in different spoken words | English sounds are recognised in different spoken words | | |
| | | (c) Identify words with the same last sounds (rhyming) and words with the same first sound (alliteration) | Words with the same last sounds (rhyming) and words with the same first words (alliteration) are identified | | |
| | | (d) Blend letter sounds to form words | Letter sounds are blended to form words | | |
| | | (e) Associate letter names with sounds | Letter names are associated with sounds | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (f) Recognise numbers and talk about times of the day | Numbers are recognized and times of the day are expressed | | |
| | 3.3 Communicate in different contexts | (a) Introduce oneself and others | One introduces himself/herself and others | Real objects, pictures, word lists, wall charts, audial/audio-visual materials | 10 |
| | | (b) Use common greetings and polite expressions | Common greetings and polite expressions are used | | |
| | | (c) Say goodbye to others | One says goodbye to others | | |
| 4.0 Kuhesabu | 4.1Kutambua dhana ya namba | (a) Kubaini dhana ya namba kwa kutumia vitu katika mazingira | Dhana ya namba kwa kutumia vitu katika mazingira imebainishwa | Video zinazojenga dhana ya namba, vitu halisi, kadi za namba, kibao fumbo, sinia la namba, chati ya namba, abakasi | 29 |
| | | (b) Kubaini namba kuanzia 1-100 kwa tarakimu na maneno | Namba kuanzia 1-100 kwa tarakimu na maneno zimebainishwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kupanga namba kwa mfuatano 1-100 | Namba kwa mfuatano 1-100 zimepangwa | | |
| | 4.2 Kutumia matendo ya kihisabati | (a) Kutambua namba katika makumi na mamoja | Namba katika makumi na mamoja zimetambuliwa | Video zinazohusu matendo ya namba, vitu halisi, kadi za namba, kibao fumbo, sinia la namba, chati ya namba na abakasi | 38 |
| | | (b) Kutumia vitu/TEHAMA kumudu dhana ya kujumlisha | Dhana ya kujumlisha imejengwa kwa kutumia vitu/TEHEMA | | |
| | | (c) Kujumlisha namba kupata jumla isiyozidi 99 | Namba zimejumlishwa kupata jumla isiyozidi 99 | | |
| | | (d) Kutumia vitu/TEHAMA kumudu dhana ya kutoa | Dhana ya kutoa imejengwa kwa kutumia vitu/ TEHEMA | | |
| | | (e) Kutoa namba zisizozidi 99 | Namba zimetolewa kwa idadi zisizozidi 99 | | |
| | 4.3 Kutumia dhana za kihisabati | (a) Kubaini maumbo ya msingi | Maumbo ya msingi yamebainishwa | Video zinazohusu maumbo yaliyorekodiwa, vitu halisi, kadi na chati za picha za maumbo | 29 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 5.0 Kuthamini utamaduni, sanaa na michezo | 5.1 Kuthamini utamaduni wake na wa watu wengine | (a) Kubaini vyakula vya Kitanzania | Vyakula vya Kitanzania vimebainishwa | Sanaa na michezo iliyorekodiwa, vitu halisi, vifani mbalimbali, chati za picha zinazoonesha vyakula, mavazi, ngoma za Kitanzania zilizorekodiwa, ngoma na filimbi | 8 |
| | | (b) Kubaini mavazi ya Kitanzania | Mavazi ya Kitanzania yamebainishwa | | |
| | | (c) Kucheza ngoma na kuimba nyimbo za asili | Ngoma na nyimbo za asili zimechezwa na kuimbwa | | |
| | 5.2[1] *** Kuheshimu tofauti za kiimani | (a) Kueleza imani za watu wanaomzunguka | Ameelezea imani za watu wanaomzunguka | | 8 |
| | | (b) Kushirikiana katika shughuli za kijamii | Shughuli za kijamii zimefanyika kwa kushirikiana | | |
| | 5.3 Kuonesha matendo yenye kimaadili | (a) Kutenda matendo yenye kimaadili | Matendo ya kimaadili yametendwa | Matendo yenye maadili yaliyorekodiwa, kadi za picha zinazoonesha kuthamini watu wengine na chati za sheria mbalimbali mfano sheria za shule | 8 |

1 ***Umahiri mahususi huu wa 5.2 utafundishwa na viongozi wa imani husika katika kipindi cha dini

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kutenda matendo yanayoonesha kuthamini watu wengine | Matendo yanayoonesha kuthamini watu wengine yametendwa | | |
| | 5.4 Kubuni kazi za sanaa | (a) Kusuka, kufinyanga, kuchora, kupiga chapa, kutunga vitu na kupaka rangi | Amesuka, amefinyanga, amechora, amepiga chapa, ametunga vitu na amepaka rangi | Kazi za sanaa zilizorekodiwa, vitu halisi na chati za picha zinazoonesha watu wakisuka, kufinyanga, kutunga vitu, kupaka rangi, kuimba nyimbo na mashairi yaliyorekodiwa | 16 |
| | | (b) Kuimba nyimbo na mashairi | Nyimbo na mashairi zimeimbwa | | |
| | | (c) Kucheza ngoma na muziki | Ngoma na muziki imechezwa | | |
| | 5.5 Kushiriki katika michezo mbalimbali | Kufanya mazoezi sahili ya viungo (*wepesi, msawazo* na *uratibu wa mwili*) | Mazoezi sahili ya viungo yamefanyika | Vitu halisi, chati za picha, na michezo sahili iliyorekodiwa | 10 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 6.0 Kutunza afya na mazingira | 6.1 Kutunza afya yake na jamii inayomzunguka | (a) Kusafisha mwili wake | Mwili umesafishwa | Vitu halisi, chati za picha, na video zinazoonesha michezo sahili, vifaa halisi vya kusafishia mwili na mavazi, chati za picha zinazohusu usafi wa mwili na mavazi, video zinazohusu utunzaji wa afya | 7 |
| | | (b) Kutunza mavazi yake | Mavazi yametunzwa | | |
| | 6.2 Kujilinda na mazingira hatarishi | (a) Kuepuka mazingira na vitu hatarishi | Mazingira na vitu hatarishi vimeepukwa | Chati ya alama za usalama, picha za wanyama, matukio na maeneo hatarishi, mazigira hatarishi na alama za usalama barabarani zilizorekodiwa na katika mazingira | 10 |
| | | (b) Kubaini alama za usalama barabarani na katika mazingira yake | Alama za usalama barabarani na katika mazingira yake zimebainishwa | | |

## Darasa la II

**Jedwali Na. 4:** *Maudhui ya Darasa la II*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kusoma | 1.1 Kutambua sauti za herufi | (a) Kubaini sauti katika maneno | Sauti katika maneno zimebainishwa | Vitu halisi, kadi na chati za picha, herufi, silabi, maneno na video zinazohusu sauti za herufi za konsonanti mwambatano na irabu kusoma silabi | 98 |
| | | (b) Kuunganisha sauti za herufi za konsonanti mwambatano (gh, ng', nz, nj, sw, bw, gw, tw, dh, pw, vy, fy, my, ml, ky, py, ft, lw) na irabu kusoma silabi | Sauti za herufi za konsonanti mwambatano (gh, ng', nz, nj, sw, bw, gw, tw, dh, pw, vy, fy, my, ml, ky, py, ft, lw) na irabu zimeunganishwa na silabi zimesomwa | | |
| | | (c) Kutamka maneno yenye silabi mwambatano | Maneno yenye silabi mwambatano yametamkwa | | |
| | | (d) Kutambua sauti zinazounda maneno katika sentensi | Sauti zinazounda maneno katika sentensi zimetambuliwa | | |
| | 1.2 Kutambua uhusiano wa sauti na herufi | (a) Kuunganisha sauti za herufi mwambatano zenye konsonanti mbili na irabu ili kuunda silabi (gh, ng', nz, nj, sw, bw, gw, tw, | Sauti za herufi mwambatano zenye konsonanti mbili na irabu zimeunganishwa ili kuunda silabi (gh, ng', nz, nj, sw, bw, gw, tw, | Vitu halisi, kadi na chati za picha, herufi, silabi, maneno na video zenye sauti za herufi mwambatano zenye konsonanti mbili na irabu | 98 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | dh, pw, vy, fy, my, ml, ky, py, ft, lw) na kutambulisha herufi mwambatano zenye maneno ya kukopa (bl, sp, sk, pt, st, ks, kt, pl, al, ar) | dh, pw, vy, fy, my, ml, ky, py, ft, lw) na herufi mwambatano zenye maneno ya kukopa (bl, sp, sk, pt, st, ks, kt, pl, al, ar) zimetambulishwa | | |
| | | (b) Kuunganisha silabi kusoma maneno yenye konsonanti tatu na irabu (njwa, nywe, shwa, ngwa, mbwe, ndwa, ng'we) | Silabi zimeunganishwa kusoma maneno yenye konsonanti tatu na irabu (njwa, nywe, shwa, ngwa, mbwe, ndwa, ng'we) | | |
| | | (c) Kuunganisha maneno kusoma sentensi | Maneno yameunganishwa kusoma sentensi | | |
| | 1.3 Kusoma kwa ufasaha | (a) Kusoma kwa kujiamini kifungu cha habari/hadithi linganifu kwa kuzingatia matamshi sahihi ya maneno | Kifungu cha habari/ hadithi linganifu kwa kuzingatia matamshi sahihi ya maneno kimesomwa kwa kujiamini | Matini zilizorekodiwa | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kusoma kifungu cha habari/ hadithi linganifu kwa kasi stahiki (maneno 50 kwa dakika) | Kifungu cha habari/ hadithi linganifu kwa kasi stahiki (maneno 50 kwa dakika) kimesomwa | | |
| | | (c) Kusoma kwa kujiamini kifungu linganifu cha habari/ hadithi kwa hisia na kwa kuzingatia alama za uandishi (nukta, mkato, alama ya kuuliza, alama ya mshangao) | Kifungu linganifu cha habari/hadithi kwa hisia na kwa kuzingatia alama za uandishi (nukta, mkato, alama ya kuuliza, alama ya mshangao) kimesomwa kwa kujiamini | | |
| | | (d) Kusoma kwa sauti kifungu cha habari/hadithi sahili | Kifungu cha habari/ hadithi sahili kimesomwa kwa sauti | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.4 Kusoma na kusikiliza kwa ufahamu | (a) Kutafsiri na kuelezea matukio (Kupanga na kusoma sentensi kwa kufuata mtiririko sahihi wa matukio, kusoma sentensi zenye mtiririko sahihi, kupanga na kusoma sentensi zilizochanganywa ili kuleta mtiririko wenye mantiki) | Matukio yametafsiriwa na kuelezewa (kupanga na kusoma sentensi kwa kufuata mtiririko sahihi wa matukio, kusoma sentensi zenye mtiririko sahihi, kupanga na kusoma sentensi zilizochanganywa ili kuleta mtiririko wenye mantiki) | Picha za matukio, kadi za sentensi, video zinazohusu kusoma na kusikiliza kwa ufahamu na matini zilizorekodiwa | 58 |
| | | (b) Kusimulia matini fupi aliyoisoma kwa mtiririko wa matukio yenye mantiki | Matini fupi zimesomwa kwa mtiririko wa matukio yenye mantiki | | |
| | | (c) Kusikiliza matini sahili kwa ufahamu | Matini sahili imesikilizwa kwa ufahamu | | |
| | | (d) Kusoma matini sahili kwa ufahamu | Matini sahili imesomwa kwa ufahamu | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kuandika | 2.1 Kutumia kanuni za uandishi | (a) Kutumia alama za uandishi (kuandika habari fupi kwa kuzingatia alama za uandishi, kuandika insha fupi kwa kuzingatia alama za uandishi, kubaini alama za uandishi zinazokosekana katika matini) | Alama za uandishi zimetumika | Video zinazohusu kanuni za uandishi na matini zilizorekodiwa zinazohusu kanuni za uandishi | 195 |
| | | (b) Kuandika mwandiko wa chapa wenye kikonyo | Mwandiko wa chapa wenye kikonyo umeandikwa | | |
| | | (c) Kuandika matini fupi kwa mtiririko wa matukio wenye mantiki | Matini fupi imeaandikwa kwa mtiririko wa matukio wenye mantiki | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 Demonstrate mastery of basic English language skills | 3.1 Develop listening and speaking skills in different contexts | (a) Use singular and plural forms of names of objects found in the environment | Singular and plural forms of names of objects found in the immediate environment are used | Books, real objects, pictures, word lists, wall charts, audial/audio-visual materials, drawing papers and coloured pens/chalks | 87 |
| | | (b) Listen and respond to simple sentences | Questions on simple sentences are answered | | |
| | 3.2 Develop early Literacy and numeracy skills | (a) Manipulate phonemes (delete, add and substute) phonemes (sounds) to form new words | Phonemes are manipulated to form new words (delete, add and substute) | Books, real objects, pictures, word lists, wall charts, audial/audio-visual materials | 147 |
| | | (b) Pronounce English sounds in written words | English sounds in different written words are pronounced | | |
| | | (c) Read and write simple English words (e.g. bag, ten, did, dog, sun) | Simple English words are read and written | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Read words with two consonant clusters (e.g. bl, cl, fl, gl, pl, sl, br, cr, dr, fr, gr, pr, tr, sc, sk, sm, sn, sp, st, and tw) and words with consonant digraphs (e.g. th, ch, sh, ph) | Words with two consonant clusters (e.g. bl, cl, fl, gl, pl, sl, br, cr, dr, fr, gr, pr, tr, sc, sk, sm, sn, sp, st, and tw) and words with consonant digraphs (e.g. th, ch, sh, ph) are read | | |
| | | (e) Read and write simple sentences | Simple sentences are read and written | | |
| | | (f) Use basic punctuation marks in sentences (target: full stop, comma and question mark) | Basic punctuation marks are used in sentences | | |
| | | (g) Express days of the week and months of the year | Days of the week and months of the year are expressed | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 4.0 Kuhesabu | 4.1 Kutumia matendo ya kihisabati | (a) Kutambua namba katika mamia | Namba katika mamia zimetambuliwa | Vitu halisi, kadi za namba, kibao fumbo, sinia la namba, chati ya namba, abakasi, Video zinazohusu matendo ya kihisabati na matini zinazohusu matendo ya kihisabati zilizorekodiwa | 173 |
| | | (b) Kujumlisha namba kupata jumla isiyozidi 999 | Namba zimejumlishwa kupata jumla isiyozidi 999 | | |
| | | (c) Kutoa namba zisizozidi 999 | Namba zisizozidi 999 zimetolewa | | |
| | | (d) Kutumia vitu/ TEHAMA kumudu dhana ya kuzidisha kama kujumlisha makundi yanayolingana | Kumudu dhana ya kuzidisha kama kujumlisha makundi yanayolingana kwa kutumia vitu/TEHAMA imejegwa | | |
| | | (e) Kuzidisha namba kwa tarakimu moja kupata zao lisilozidi 100 | Namba kwa tarakimu moja imezidishwa kupata zao lisilozidi 100 | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (f) Kutumia vitu/TEHAMA kumudu dhana ya kugawanya kama kutoa makundi yanayolingana | Dhana ya kugawanya kama kutoa makundi yanayolingana kwa kutumia vitu/TEHAMA imejengwa | | |
| | | (g) Kugawanya namba zisizozidi 100 bila baki | Namba zisizozidi 100 zimegawanywa bila baki | | |
| | 4.2 Kutumia dhana za kihisabati | (a) Kubaini dhana ya sehemu kwa kutumia vitu halisi na TEHAMA (nzima, nusu, robo, theluthi, theluthi mbili n.k) | Dhana ya sehemu kwa kutumia vitu halisi na TEHAMA (nzima, nusu, robo, theluthi, theluthi mbili n.k) imebainishwa | Vitu halisi, kadi na chati za picha na video zinazohusu dhana ya sehemu | 100 |
| | | (b) Kuonesha sehemu kwa kutumia namba ( $\frac{1}{4}$, $\frac{1}{2}$ n.k) | Sehemu kwa kutumia namba ( $\frac{1}{4}$, $\frac{1}{2}$ n.k) imeoneshwa | | |
| | | (c) Kutumia stadi za vipimo katika miktadha mbalimbali | Stadi za vipimo katika miktadha mbalimbali zimetumika | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kutumia maumbo ya msingi kuumba maumbo mbalimbali | Maumbo ya msingi kuumba maumbo mbalimbali yametumika | | |
| 5.0 Kuthamini utamaduni, sanaa na michezo | 5.1 Kuthamini utamaduni wake na wa watu wengine | (a) Kubaini makazi ya asili ya Kitanzania | Makazi ya asili ya Kitanzania yamebainishwa | Kadi na chati za picha na video zinazohusu utamaduni, sanaa na michezo | 10 |
| | | (b) Kubaini shughuli mbalimbali za jamii za Kitanzania | Shughuli mbalimbali za jamii za Kitanzania zimebainishwa | | |
| | 5.2***[2]Kuheshimu tofauti za kiimani | (a) Kuhusianisha imani na maadili mema | Amehusianisha imani na maadili mema | | 10 |
| | | (b) Kujali matendo ya imani za watu wengine | Amejali matendo ya imani za watu wengine | | |

2 ***Umahiri mahususi huu wa 5.2 utafundishwa na viongozi wa imani husika katika kipindi cha dini

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 5.3 Kubuni kazi za sanaa | (a) Kushiriki katika sanaa za utendaji wa mikono (kufuma, kufinyanga, kuchonga, kushona, kutia nakshi) | Ameshiriki katika sanaa za utendaji wa mikono (kufuma, kufinyanga, kuchonga, kushona, kutia nakshi | Kadi, chati za picha na kazi za sanaa zilizorekodiwa | 22 |
| | | (b) Kushiriki katika sanaa za ubunifu wa sauti (ngonjera, majigambo, vichekesho) | Ameshiriki kufanya sanaa za ubunifu wa sauti (ngonjera, majigambo, vichekesho) | | |
| | | (c) Kufanya sanaa zinazohusisha utendaji wa mwili (kuigiza, mijongeo ya mwili) | Sanaa zinazohusisha utendaji wa mwili (kuigiza, mijongeo ya mwili) zimefanyika | | |
| | 5.4 Kushiriki katika michezo mbalimbali | Kucheza michezo sahili | Michezo sahili imechezwa | Vitu halisi na michezo sahili iliyorekodiwa | 16 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 6.0 Kutunza afya na mazingira | 6.1 Kuchunguza vitu vilivyopo katika mazingira | Kufanya uchunguzi sahili wa viumbe hai na visivyo hai katika mazingira yanayomzunguka | Uchunguzi sahili wa viumbe hai na visivyo hai umefanywa | Picha, vitu halisi na video zinazohusu kuchunguza vitu vilivyopo | 26 |
| | 6.2 Kujilinda na mazingira hatarishi | Kuzingatia alama za usalama barabarani na katika mazingira yake | Alama za usalama barabarani na katika mazingira yake zimezingatiwa | Picha, vitu halisi na mazingira hatarishi yaliyorekodiwa | 19 |
| | 6.3 Kuwa na mtazamo chanya kuhusu mazingira | Kushiriki katika shughuli zinazohusu mazingira shuleni | Ameshiriki katika shughuli zinazohusu mazingira shuleni | Kadi na chati ya picha, vitu halisi na matini zinazohusu mazingira zilizorekodiwa | 19 |

## Bibliografia


Budgell, G & Ruttle, K. (2015). *Cambridge primary english*. Cambridge University Press.

Collins, H. (2011). *Easy learning english vocabulary*. Harper Collins.

Crichton, J & Koster, P. (2006). *English made easy*. Tuttle Publishing.

Hallwell, S. (1992). *Teaching english in the primary classrooms*. Longman.

Herring, P. (2016). *Complete english grammar rules*. FARLEX International.

Mauritius Institute of Education (2005). *National curriculum framework, grades 1 to 6.* Republic of Mauritius.

Ministry of Education and Vocational Training. (2014). *Education and training policy*. MoEC.

Ministry of Education, Science and Technology. (2019). *English language syllabus for primary education.* Ministry of education Science and Technology.

Ministry of Education. (2003). *Zambia basic syllabi grades 1-7.* Ministry of Education.

Murphy, R. (2007). *Essential grammar in use (3rd ed).* Cambridge University Press.

Murphy, R. (2019). *English grammar in use (5th ed.).* Vivar Printing.

Persekutuan, P. P. K. (2013). *Malaysia education blueprint 2013-2025 (Preschool to Post-Secondary Education)*. Putrajaya: Kementerian Pendidikan Malaysia.

Random, P. (2016). *English for Everyone.* Penguin Random House.

Seaton, A. & Mew, Y.H. (2007). *Basic english grammar for english language leaners.* Saddleback Educational.

Republic of Kenya, (2019). *Basic education curriculum framework nurturing every learner's potential.* Kenya Institute of Curriculum Development.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2022*). Ripoti ya maoni ya wadau kuhusu uboreshaji wa mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

The United Republic of Tanzania (2019). *National curriculum framework for basic and teacher education*. Ministry of Education, Science and Technology.